

102/3
KISWAHILI
Karatasi ya3
(FASIHI)
JULAI / AGOSTI - 2010
MUDA: SAA 2 ½

TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA BURETI - 2010
Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari Kenya (KCSE)

102/3
KISWAHILI
Karatasi ya 3
(FASIHI)
JULAI / AGOSTI - 2010
MUDA: SAA 2 ½

MAAGIZO

- ❖ Jibu maswali manne pekee
- ❖ Swali la kwanza ni la lazima
- ❖ Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja
- ❖ Jibu maswali matatu yaliyobaki kutoka sehemu zilizobaki yaani tamthilia, Riwaya, Hadithi fupi na Ushairi.

Karatasi hii ina kurasa 4 zilizopigwa chapa
Watahiniwa wanastahili kuona kuwa maswali yote yako na hakuna yaliyoachwa.

TAMTHILIA

KITHAKA WA MBERIA: KIFO KISIMANI

LAZIMA

1. “.....ni nini kitakachokuwa utu wako....”
 - (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
 - (b) Kulingana na mnenaji ni nini faida ya utu wa mtu. (alama 6)
 - (c) Kwa kutoa mifano maridhawa eleza jinsi vijana wamethibitisha uzalendo wao. (alama 10)

RIWAYA:

UTENGANO - Said A Mohamed

2. “.Hakuweza kuzizuia hisia zake, alilia taratibu kwanza, halafu sauti ilizidi kuwa kubwa, akalia kwa kwikwi. . .
 - (a) weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
 - (b) Onyeshajinsi anayerejelewa anaendeleza maudhui ya mabadiliko. (alama 8)
 - (c) “Msiba wa kujitakia hauna kilio” Thibitisha ukweli huu ukirejelea Anayerejelewa kwenye dondoo hili. (alama 8)
- au**
3. Mtunzi wa riwaya ya utengano amebobea katika matumizi ya mbinu za jazanda na taswira. Tetea kauli hii. (alama 20)

HADITHI FUPI

4. Watunzi wa hadithi za mayai waziri wa maradhi wamefaulu kushughulikia maswa!a ibuka katika jamii zetu. Jadili ukizingatia.
 - (i) Mkimbizi
 - (ii) Ndimi za mauti
 - (iii) Fumbo la mwana
 - (iv) Pwaguzi (alama 20)
- au**
5. Onyeshajinsi rntunzi wa hadithi “Msamaria Mwema” ameshughulikia maudhui yafuatayo.
 - (i) Utabaka.
 - (ii) Kutowajibika kwa viongozi. (alama 20)

FASIHI SIMULIZI

6. (a) Popoo wawili wavuka ng'ambo.
- (i) Hiki ni kipera gani katika fasihi simulizi?
- (ii) Eleza aina tatu za kipera hiki. (alama 6)
- (iii) Bainisha matumizi matatu ya lugha katika kipera hiki huku ukitoa mifano.(alama6)
- (b) (i) Kitangulizi cha hadithi kina umuhimu gani? Eleza umuhimu tatu. (alama 3)
- (ii) Eleza sifa nne bainifu za hadithi za fasihi simulizi. (alama 4)

USHAIRI

7. Soma mashairi yafuatayo kisha ujibu maswali.

Shairi A

Nimeona, milima na mabonde, misitu na nyika.
Nimeona, majanj na umande, uliotandazika
Nimeona, mkulima yuwenda shambani

Nimeona, uwanda na magugu, yalomkabili.
Nimeona, wajibu na vurugu, 'wiano mkali
Nimeona, mkulima akiwa tayari.

Nimeona, kwa ari na juhudi, anatupa jembe
Nimeona, kakaza ukaidi, kwa nguvu achimbe
Nimeona, mkulima akiwa kazini.

Nimeona, kijua kinawaka,kama jahanamu!
Nimeona, jembe lainuka, linapohujumu
Nimeona, mkulima akiwa mbioni.

Nimeona, mvua yamiminjka, naye -hatohisi
Nimeona, kwa kani anatimka, bila wasiwasi
Nimeona, mkulima akiwa kazini.

Na sioni, jasho linapomwaika, yendapo mazao
Na sioni, hadhiye kutukuka, ila kilio
Kwa nini? Nauliza mkulirna; Kwani?

Shairi B

Wakati miaka inaibwa mmoja mmoja
Kurudi nyuma, kusimama, kupunguza mwendo
Siwezi kama gurudumu nitajiviringisha
Mtelemko mkali huu.

Lini na wapi mwisho sijui:

Mbele chui mweusi, nyuma mwanga
Nionako kwa huzuni vifurushi maelfu vya
dhambi.

Kisu, maisha kafiri haya
Kama kutazama nyuma au mbele
Ni kufa moyo mzima!

Sasa kama Simba-Mtu shauri nimekata.
Ya nyuma sana nisija li ya mbele sana
niyakabili
Kwa ujasiri na uangalifu nitazunguka
Nikifuata kamba kama ng'ombe aliyefungwa,
Kila mpigo Wa moyo wangu
Huu mpigo muziki wa maisha

- (a) Onyesha tofauti zinazodhihirika katika mashairi haya kwa upande wa umbo. (alama 4)
- (b) Fafanua mtindo wa haya mashairi. (alama 3)
- (c) Andika ubeti wa sita katika shairi A kwa lugha nathari (alama 3)
- (d) Thibitisha matumizi ya idhini ya Mshairi katika tungo hizi (alama 3)
- (e) Chambua maudhui ya tungo hizi kwa kutolea mifano. (alama 3)
- (f) **Eleza maana ya mafungu ya maneno haya kama yalivyotumiwa**
- (i) Kakaza ukaidi
- (ii) Simba - Mtu (alama 2)

